# HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA.

SHULE YA SEKONDARI LUGUFU GIRLS
S.L.P. 12
UVINZA – KIGOMA
Mkuu wa shule: 0767505902
Makamu wa shule: 0714935998
Mtaaluma wa shule: 0752446138
Mwalimu wa nidhamu:0659586726
Email: lugufugirls@gmail.com
Website: lugufugirlsschoo.ac.tz

KUMB. LGSS/2018/5
MZAZI/MLEZI WA ……..……
……..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2018.**

Ninafurahi Kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (form v) katika shule ya sekondari LUGUFU GIRLS, baada ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne.
Shule ya sekondari Lugufu girls iliyopo karibu na makao makuu ya Wilaya ya Uvinza eneo la Lugufu, shule ipo umbali wa kilometa 11 kusini kutoka makao makuu ya Wilaya.kwa wanaopitia njia ya tabora kituo cha kushukia kinaitwa LUGUFU POLISI kilometa 2 kutoka makao makuu ya wilaya ukishuka utachukua bodaboda ni Tshs 4000 hadi shuleni
Kwa wanaopitia njia ya kibondo-kasulu kuna njia mbili,
Njia ya kwanza ni kushuka kasulu unapanda gari zinazokuja uvinza nauli ni 6000 ukishuka stendi ya Uvinza unapanda gari zinazoelekea Kigoma mjini nauli ni Tshs 2000 mpaka kituo cha LUGUFU POLISI, ukishuka utachukua bodaboda Tshs 4000 hadi shuleni
Njia ya pili ni ya kwenda moja kwa moja hadi Kigoma mjini ukishuka stendi unapanda gari zinazo elekea UVINZA nauli ni Tshs 4000 utashuka kituo kinachoitwa LUGUFU POLISI ukishuka unachukua bodaboda Tshs 4000 hadi shuleni
Kwa wanaokuja na usafiri wa Tren utashuka stesheni ya UVINZA utachukua bodaboda kwa Tshs 1000 hadi kituo cha daladala utapanda gari zinazoelekea Kigoma mjini nauli ni Tshs 2000 utashuka kituo cha LUGUFU POLISI kisha utachukua bodaboda kwa Tshs 4000 hadi shuleni.
Kwa wanaokuja na usafiri wa ndege utashukia Kigoma mjini utapanda gari za kwenda UVINZA nauli ni Tshs 4000 utashuka kituo cha LUGUFU POLISI utachukua bodaboda kwa Tshs 4000 hadi shuleni.
Mda wa kuripoti ni kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO.**

Unapokuja shuleni unatakiwa kuja na vitu vifuatavyo:-

(i) Ada Tshs. 35,000/= kwa muhula au Tshs. 70,000/= kwa mwaka (Mwanafunzi asiyelipa ada hataruhusiwa kuendelea na masomo)
(ii) Fedha kwa ajili ya tahadhari TShs. 5,000/=
(iii) Rimu moja ya karatasi (A4) isiyo na mistari ni kwa kila mwaka
(iv) Fedha kwa ajili ya kitambulisho na picha Tshs. 6,000/=
(v) Fedha kwa ajili ya taaluma Tshs. 10,000/= kwa muhula mmoja au Tshs. 20,000/= kwa mwaka.
(vi) FedhaTshs.30000/= kwa ajili ya ulinzi,wapishi na wafanyakazi wengine
(vii) Fedha kwa ajili ya nembo Tshs. 2,000/=
(viii) Fedha kwa ajili ya ukarabati wa samani ni 15,000/=
(ix) 10000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs 5000/= na ya bima ya afya Tshs 5000/=.
(x) Shilling 20000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima
(xi) Aje na Result slip na cheti cha kuzaliwa Orginal na nakala ya kubaki shuleni
(xii) Jumla ya michango kwa mwaka ni Tshs 178,000/= na nusu muhula ni Tshs 118,000/= na muhula wa pili ni Tshs 62,000/=

**VIFAA VYA MASOMO.**

(i) Daftari Tisa (9) kubwa kuanzia 3quire (counter book at least 3 quire) kwa michepuo ya HGK, HGL, HKL, HGE na Daftari 11 kwa PCB na CBG.
(ii) Kalamu za risasi
(iii) Kalamu za wino za kutosha (bluu na nyeusi)
(iv) Mkebe wa hisabati (mathematical set), Rula
(v) Kamusi ya Kiswahili sanifu moja (1) kwa wanafunzi wa Michepuo ya HKL na HGK na English for Advanced learners Dictionary moja (1) kwa michepuo yote.
(vi) Uje na vitabu vinavyohusisha masomo yako vyote bila kukosa.
(vii) Scientific calculator kwa michepuo ya HGK, HGE, PCB, CBG,na HGL
(viii) Graphy pad 1 kwa CBG,PCB,HGL,HGK na HGE
(ix) Koti ya maabara na disseting kit &dissecting guide (manual) kwa wanafunzi wa PCB na CBG

**SARE ZA SHULE**

(i) Sketi nyeusi mbili kitambaa kisicho cha mterezo/kitambaa cha suti zenye
Linda box mbele moja na nyuma moja ziwe kubwa na kulia 2 kushoto 2 ndogo ndogo, sketi iwe ndefu chini ya magoti na tai nyeusi ndefu kwa wanafunzi wa kikristo na kiislam.
(ii) Shati mbili nyeupe mikono mirefu
(iii) Viatu vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi
(iv) Soksi ndefu rangi nyeupe pair mbili 2

(v) Sweater la kijani ya kijeshi {dark green}, lenye michirizi myeusi miwili mwishoni mwa kila mkono, kuzunguka shingo, chini mwishoni mwa sweater na mistari myeusi miwili mikubwa kifuani.

(vi) Sketi moja ya kushindia (shamba dress)rangi ya zambarau yenye malinda

(vii) T-shirt ya shule rangi ya kijani, yenye kola na michirizi myeusi mwishoni mwa kila mkono na kuzunguka kola. Yenye nembo ya shule kifuani na motto wa shule mgongoni.

**(viii)** Ijabu nyeupe kwa ajili ya darasan na Ijabu ya zambarau ya kushindia ambayo ni ndefu ya kufunika mikono.

**(ix)** Track suti nyeusi yenye michirizi myeupe pembeni kwa ajili ya baridi mda wa usiku.

**(x)** Sketi za kushindia mbili {2} rangi ya zambarau. Kitambaa chochote ila kisiwe cha kung'aa

**SARE ZA MICHEZO**

(xi) Fulana ya bluu isiyo na maandishi

(xii) Raba nyeupe au nyeusi za michezo

**(xiii)** Bukta nyeusi yenye michirizi myeupe

**VIFAA VYA BWENINI.**

(i) Shuka mbili (2) rangi ya pink na branket moja (1)

(ii) Sahani moja (1) bakuli moja (1) na kijiko (1)

(iii) Ndoo moja ya lita kumi na beseni 1 ya kufuria

(iv) Kidumu cha lita 5 au chombo chochote kisafi kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa

(v) Reki moja (1) yenye mpini.

(vi) Kwanja moja (1)

(vii) Godoro moja (1) futi 2 ½

(viii) Fagio moja (1) wa chelewa

(ix) Mopa au fagio la kusugulia

(x) T-shirt zaidi ya moja za bluu zisizokuwa na maandishi za kushindia

**MUHIMU KWA WOTE.**

(a) Sare zote zitakaguliwa ipasavyo pamoja na maagizo mengine pindi mwanafunzi anaporipoti shule. Usipotimiza maagizo haya utarudishwa nyumbani mara moja. Pia haturuhusu nguo/mavazi yasiyo sare za shule.

(b) Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya shule:

(c) Namba ya akauti (Acount Number): 51601100089

Benki (Bank): NMB-KIGOMA BRANCH

Jina la Akaunti (Account Name) Lugufu Girls Secondary School

**UTAWALA**

Mzazi yeyote yule alete vithibitisho vya mtoto wake endapo atakuwa na matatizo yanayohusiana na afya ya mtoto husika.

**MENGINEYO**

(a) Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shuleni zaidi ya siku 90 mfululizo za masomo bila taarifa yoyote ya kiofisi atakuwa amejiachisha shule kwa hiyari yeye mwenyewe. Hii ni kutokana na sheria za Elimu EDG. A3/60 ya mwaka 1985.

(b) Shule itafunguliwa rasmi kwa muhula wa kwanza tarehe 01/07/2018 saa 1 asubuhi. Unatakiwa kuripoti siku hiyo kwa ajili ya Orientation Course.

**KIAMBATANISHO A:**

1. **SHERIA ZA SHULE**

- Utatakiwa kuzingatia na kufuata vyema sheria za shule.
- Utatakiwa kuonyesha nidhamu kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzako.
- Mwalimu anapopita mwanafunzi asimame na kusalimia kwa lugha ya kiingereza.
- Utalazimika kuzungumza lugha ya kiingereza wakati wote shuleni.
- Ni mwiko mwanafunzi kutumia lugha ya kihuni au matusi.
- Utatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, picha ya rais wa jamuhuri ya muungano wa Tanzania, wimbo wa taifa na katiba ya Nchi.
- Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni.

**2. UTII**

- Mwanafunzi atakuwa mtiifu kwa wanafunzi na viranja wa shule.
- Mwanafunzi atatekeleza amri ya mwalimu bila ubishi.
- Mwanafunzi atatakiwa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa.

**3. SEHEMU ZILIZOKATAZWA**

**Mwanafunzi haruhusiwi kuingia sehemu zifuatazo;**

- Guest house na kumbi za starehe.
- Sehemu za kuuzia pombe (vilabu vya pombe, baa n.k ).
- Nyumba za walimu.
- Maabara isipokuwa kwa kibali maalumu.

**4. HIVYO NI KOSA KWA MWANAFUNZI**

- Kuanzisha/kushiriki kwenye mgomo, fujo au ukaidi wa aina yoyote.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, picha za viongozi wa chama na serikali na bendera ya taifa.
- Kuiba.
- Kuwa mwasherati.
- Kutumia kileo au pombe ya aina yoyote ile.
- Kuvuta sigara, bangi n.k.
- Kupatikana na makosa ya jinai.
- Kubeba mimba au kutoa mimba.
- Kuolewa.
- Kupigana.
- Kuwa mtoro au mchelewaji.
- Kuwa mvivu darasani au nje ya darasa.
- Kusema uongo.
- Kuvaa mapambo ya aina yeyote ile, mfano pete, mkufu, heleni n.k.
- Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi.
- Kundharau bendera ya Taifa.
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- Kwa body sprays, mwanafunzi anaruhusiwa kuwa na body spray yeyote ambayo ina nembo ya **smart collection** tu pamoja na **lovellea sprays**.

**Endapo utavunja sheria mojawapo kati ya hizo zilizotajwa hapo juu, utapewa adhabu zifuatazo kulingana na kosa.**

- **KUCHAPWA VIBOKO VISIVYOZIDI VINNE (4) KWA AWAMU MOJA KWA KOSA.**
- **KUFANYA KAZI NGUMU KAMA KUCHIMBA SHIMO LA TAKATAKA N.K.**
- **KUPEWA ONYO KALI LA MAANDISHI.**
- **KUSIMAMISHWA SHULE KWA MUDA.**
- **KUFUKUZWA SHULE.**

**Karibu sana shule ya sekondari lugufu girls,**
**You are warmly welcome at lugufu girls secondary school.**

.

Nakala: Mkaguzi wa shule
Kanda ya Ziwa Magharibi
S.L.P. 1185

**Kigoma**

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza
S.L.P. 12
**Uvinza – Kigoma**

**…….**
**Mkuu wa shule**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A: From……

TO THE MEDICAL OFFICER (designation, ministry, division, station)

Mr./Mrs./Miss……
……

Please examine the above named as to his/her fitness for Appointment/reengagement as a…… insert title to post on temporary /permanent and pensionable/contract terms.

Date……. Signature……

PART B:

To be completed by medical officer

I have examined the above and consider that he/she is physically fit /unfit for appointment/re-engagement as above.

Date…….
Signature…….

Station……
Destination…….. (delete as nece

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect of all Form one/five entrants

Full
Name…….

Age……
……

Blood count (red and white)……

Stool examination……..

Urine
analysis……

Syphilis
test…….

T.B
test……
…

Ears……
……..

Chest……
…….

Spleen……
……

Abdomen……
..

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical directs or impairment(s) infection chronic of family diseases.

……
……
……
……
…….....

I certify that the above is fit to pursue as stated above

Signature……..

Destination……..

Date…….Station……
…

Note: Medical Officer: At the time of examination please treat the individual for any ailments you know.

NB:  This completed form should be sent to the school with your acceptance from or brought when you come to school.

No pupil may enroll without certificate of physical fitness

LUGUFU GIRLS SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 12 UVINZA-KIGOMA
FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi ……..liwe jina ulilolitumia katika shule uliyotoka na utalitumia kwa miaka yote utakayokuwa hapa shuleni na huruhusiwi kulibadili.

Dini……Tarehe ya kuzaliwa ……

Nambari ya kuingizwa shuleni……Shule aliyotoka ……

Tarehe……. Michezo uipendayo au shughuli uzipendazo (hobbies) ……..

Kipimo au historia ya ugonjwa ……

Unaishi na nani/uhusiano ……

Jina na anwani ya kudumu ya mzazi/mlezi atakayetumiwa ripoti ya maendeleo yako ya kitaaluma na tabia……

Kazi ya mzazi/mlezi……..

Mahali ……Wilaya …….Mkoa ……

Habari nyinginezo ……..

Mzazi /mlezi aliye hai …….

Wageni maalum wanaoruhusiwa na mzazi/mlezi wa mwanafunzi watakaomtembelea mwanafunzi awapo shuleni.

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi mwenyewe.

JINA.....

UHUSIANO.....

NO.SIMU.....

ANAKOTOKA.....

KAZI YA BABA/MAMA au MLEZI

1.....

2.....

Sahihi ya mzazi /mlezi…….tarehe…….. simu……

Mimi (jina la mwanafunzi) …….. ninaahidi kuzingatia utaratibu,Kanuni na sheria za shule bila kukiuka. Kinyume na hayo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu. Nitasoma kwa bidii na kufanya kazi ninazotakiwa ili kufikia lengo linalotakiwa

**FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAE KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LUGUFU GIRLS**

1. Mimi ……..... Baba/Mama/Mlezi wa …….. Ninayeishi Wilaya …… Mkoa…… nakubali mwanangu …..... ajiunge na shule ya sekondari ya wasichana **Lugufu Girls** katika mchepuo wa masomo…….. aliyochagua yeye mwenyewe.
2. Mimi mzazi/Mlezi wa kijana huyu naahidi kushirikiana na walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule. Kwamba ni wajibu wangu kama mzazi/mlezi kumuhimiza mwanangu asome kwa bidii na afuate sheria na taratibu zote za shule.
3. Kwamba nitalipa ada na michango mingine yote ya shule katika muda uliopangwa na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia.
4. Nakiri nimempatia/sijampatia mwanangu simu aina ya ……. wakati anakuja

EDUCATION FOR SUCCESS